SHULE YA UPILI YA ALLIANCE
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA, 2016 - KIDATO CHA NNE
JINA.....TAREHE 22/3/2016.
NAMBARI YAKO.....DARASA.....
MUDA: SAA 2 ½
KISWAHILI 102 / 2; (Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha, Isimu-Jamii)
Jibu maswali yote;
Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali. Karatasi hii ina kurasa 9. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SWALI	UPEO	ALAMA
1. Ufahamu	15	
2. Ufupisho	15	
3. Matumizi ya lugha	40	
4. Isimu Jamii	10	
Jumla	80	

UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali *(alama 15)*

Kiongozi ni mtu aliye na madaraka na wajibu wa kuwaelekeza wengine. Katika nchi hii yetu ya Kenya, kuna viongozi katika viwango tofauti tofauti. Kuna viongozi miongoni mwa wanafunzi ambao huitwa viranja. Fauka ya hao kuna viongozi wa shule ambao ni walimu wakiongozwa na Mwalimu Mkuu. Wazazi pia ni viongozi katika familia. Wakuu wa dini mbalimbali pia huitwa viongozi kwa sababu wana jukumu la kuwaongoza waumini wao. Nchin kuna viongozi katika ngazi tofautitofauti kuanzia mashinani hadi kileleni, yaani ngazi ya kitaifa. Unafiki ni hali ya kujifanya kuwa mkweli ilhali ulaghai umeshamiri.

Kiranja ni kiongozi wa wanafunzi aghalabu katika shule za msingi na za upili. Wao hupewa jukumu la kuwa macho ya walimu katika shule. Wanastahili kuhakikisha kuwa wanafunzi wenzao wanafuata sheria za shule kwa kina ili kuhakikisha kuwa nidhamu ya wanafunzi ni ya kupigiwa mfano. Viranja hawa baadaye hubahatika na kuwa viongozi katika ngazi tofauti katika nchi. Mifano ya watu waliofaulu kuwa viongozi kutokana na ushupavu wao walipokuwa viranja shuleni ni kama vile Bwana Amos Wako aliyekuwa kiranja mkuu katika shule yake ya upili na baadaye akawa mkuu wa sheria nchini Kenya kwa muda wa zaidi ya miaka kumi na minane. Sasa yeye ni seneta wa Busia. Aliyekuwa jaji mkuu wa Kenya Bwana Evans Gicheru alikuwa kiranja katika shule moja ya kitaifa nchini. Jaji wa mahakama ya juu Bwana Leonard Lenaola pia alikuwa kiranja aliyewajibikia maktaba katika shule yake ya upili. Profesa Ole Kiyiapi na bwana Mugo Kibati ni mifano tu ya viongozi waliopata tajiriba ya uongozi kutokana na ukakamavu wao kama viranja wakuu katika shule ya upili ya Alliance.

Ili kufaulu katika jukumu hili la kuongoza watu katika nchi, viongozi wanastahili kuwa na maadili na kuepuka unafiki au ulaghai wa kila aina. Ni jambo la kusikitisha kuona kiongozi

mmoja wa dini katika mji wa Nairobi akimtumia kahaba kulaghai kondoo wake Mungu. Kasisi huyo kulingana na ushuhuda wa kahaba husika, alijaribu kuwahadaa waumini kuwa alikuwa na uwezo wa kuuponya ugonjwa uliokuwa umeupinda midomo. Hata hivyo ulaghai wake uligundulika baada ya kahaba huyo kutoboa siri na kuanika peupe ulaghai unaofanywa na baadhi ya viongozi wa dini katika kujitafutia umaarufu na kupata ukwasi kutokana na ulaghai. Ama kweli siku zake za arubaini zilikuwa zimetimia.Tumewasikia pia baadhi ya makasisi kama vile Kanyari wakiwarai adinasi kupitia vyombo vya habari kupanda mbegu ili waweze kuombewa. Injili ya ufanisi imetawala katika ajenda za wahubiri ili kuwalaghai waumini wao. Imeripotiwa kuwa baadhi ya waja wamejipata wakipokea vitisho iwapo hawatatuma fulusi kiasi fulani ili kuepuka ombi la laana kutoka kwa makasisi hao laghai.

Katika ulingo wa siasa utawapata viongozi wanafiki ambao hujihusisha na mambo ya kishirikina na uchawi ili kujipatia umaarufu kisiasa. Wao husafiri katika mataifa ya nje au maeneo fulani ili kukutana na 'werevu', watakaowasaidia katika njama hii. Viongozi hawa pia huonyesha unafiki wao kwa kutoa ahadi chungu nzima katika ile hali ya kuwashawishi wapiga kura. Kinaya ni kuwa baada ya wao kuchaguliwa, ahadi hizo hutupwa katika kaburi la sahau.Wao hughuria katika miji mikuu huku wakiwasahau wananchi waliowachagua katika nyadhifa hizo. Hata hivyo unafiki wao hujitokeza baada ya miaka mitano hivi wanapowarudia wale wale wananchi na kujaribu kuwashawishi kwa mara nyingine ili wachaguliwe tena. Wao hutumia mbinu zisizofaa katika ushawishi wao ikiwemo kuwachochea raia na kuwatia wananchi hofu. Wengine husababisha machafuko baina ya raia ili kuwaogofya wapinzani au raia wanaonekana kana kwamba hawawaungi mkono katika azma zao za kuwa viongozi. Viongozi kama hawa huweza kuwahonga baadhi ya raia ili kuhakikisha kuwa wanapata kura na kunyakua uongozi kwa mara nyingine.

Mashirika ya kiserikali, wizara mbalimbali, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta za kibinafsi huhitaji viongozi walio na uajibikaji. Si ajabu kuona wizara fulani ikishindwa kutimiza baadhi ya majukumu iliyokabidhiwa kisheria kutokana na unafiki na ulaghai katika wizara hizo. Mchezaji maarufu wa soka nchini Kenya, Macdonald Mariga, anayesakata soka ya kulipwa huko ughaibuni, hivi majuzi alikosa kuiwajibikia timu ya taifa kwa sababu shirika linalohusika lilikosa kumlipa pesa alizotumia kama nauli ya ndege. Shirika la kandanda nchini lilionyesha mfano mbaya wa kutowajibikia wachezaji wanaojitolea kizalendo kuipeperusha bendera ya nchi yetu katika mchezo wa kandanda. Iwapo shirika hili linafaa kumlipa mchezaji kama huyu kisha likakosa kufanya hivyo, bila shaka tatizo liko katika uongozi wake. Tunatarajia rais mpya wa KFF Bwana Nick Mwendwa atasaidia kuboresha soka nchini. Nchi za Kiafrika zilizonawiri katika soka kama vile Nigeria, Ghana, Cameroon, Misri, Ivory Coast, na nyinginezo, huwa na uongozi wazi na dhabiti katika mashirika yanayohusiana na suala hili la kandanda. Ufanisi huu pia hushuhudiwa katika soka safi ya ligi kuu ya Uingereza ambapo timu kama vile Chelsea, Arsenal, Leicester na nyinginezo zimedhihirisha hili.

Ni jukumu la viongozi katika sekta zote za mamlaka kuhakikisha kuwa wanazingatia uwazi katika uongozi wao. Wanastahili kuepuka kutumia mbinu zisizofaa katika kuwashawishi raia ili kusalia katika nyadhifa hizo. Katika viwango mbalimbali, lazima uajibikaji uonekane. Uongozi huanza kuchipuka kuanzia shuleni na vyuoni. Inamaanisha kuwa ni

lazima viongozi katika shule hizi wajaribu iwezekanavyo kuwa kielelezo cha kuigwa na wanafunzi hawa ambao huwa viongozi wa baadaye. Uaminifu na uwazi ni sharti uzingatiwe na kila mtu anayepata nafasi ya kuwaongoza watu wengine.

Maswali

1. Kwa nini wazazi ni viongozi? (alama 2)

2. Thibitisha kuwa uongozi huanzia shuleni (alama 2)

3. Kwa nini baadhi ya viongozi hupenda kutumia ulaghai? (alama3)

4. Ni mbinu zipi nyingine ambazo viongozi hutumia ili kubaki uongozini? (alama3)

5. Uongozi wazi michezoni una manufaa gani? (alama 2)

6. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa (alama 3)

Kielelezo-
Werevu-
Ghuria-

2. **UFUPISHO**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu swali (alama 15)

Kulingana na takwimu za Shirika la Afya Ulimwenguni, takribani watu milioni moja nukta mbili, huangamia katika ajali za barabarani kila mwaka kote ulimwenguni. Nchini Kenya pekee zaidi ya watu elfu tatu huaga dunia kutokana na ajali hizi kila mwaka huku zaidi ya elfu tano wakijeruhiwa au hata kulemazwa. Usalama barabarani ni jukumu la kila insi. Watu wengi hungojea serikali ili kukabiliana na tatizo hili. Serikali haiwezi kutufanyia kila kitu. Baadhi ya mambo huhitaji sisi wenyewe kuwajibika na kujaribu kuyazuia kutumaliza. Usalama barabarani ni ile hali ya kuhakikisha kuwa barabara zetu ziko salama kwa

kutumiwa katika usafiri.Usafiri waweza kuwa wa kutumia magari, pikipiki,baiskeli,ndege,meli au miguu. Mara kwa mara tumeshuhudia watu wakiangamia katika barabara zetu. Hivi majuzi shirika la Safaricom liliamua kujitolea katika kampeni kali iitwayo,"Usinyamaze". Kusudi la kampeni hii lilikuwa ni kujaribu kupunguza maangamizi katika barabara zetu.

Kuna mambo kadha wa kadha yanayosababisha barabara zetu kukosa kuwa salama. Katika miaka ya themanini, safari ya kutoka mji wa Kitale hadi Lodwar ilikuwa sawa na kuingia jehanamu. Wahalifu walikuwa wakivamia magari na kuwaua watu. Wengine walikusudia kuwapora wasafiri mali yao. Akina mama na wasichana pia walibakwa na kutendewa matendo mengi ya kihayawani. Hata hivyo serikali iliingilia suala hili na kulainisha mambo.

Usalama wa barabara zetu pia husababishwa na madereva wasiokuwa makini katika barabara wanapyaiendesha magari. Wengine hupuuza sheria za trafiki na kisha kusababisha ajali au maangamizi. Madereva wengine huendesha magari yao kwa mwendo wa kasi kupita kiasi. Wakiwa katika mwendo huo wengi hushindwa kuyadhibiti. Mwishowe hubingiria bingiri bingiri na kupoteza maisha ya wasafiri wasio na hatia.
Barabara zilizojaa mashimo pia huchangia usalama wa barabara zetu kuzorota. Ajali nyingi hutokana na barabara mbovu. Madereva wanapojaribu kukwepa mashimo haya, wao hushindwa kukadiria umbali wa gari litokalo katika upande huo mwingine. Matokeo ni kugongana dafrau na kusababisha ajali au maangamizi. Fauka ya hayo kuna madereva ambao wanaangamiza maisha ya wasafiri wasio na haruma kwa kujaribu kupita gari lililo mbele mahali ambapo si salama. Hivi majuzi ajali mbaya sana imetokea katika eneo la Mai mahiu na kuhusisha magari manane kutokana na utepetevu wa madereva. Wao hufanya hivyo katika maeneo hatari kama vile katika milima, katika njia zilizopinda, mahali palipo na ukungu kama vile katika maeneo ya Limuru na Kimende katika barabara kuu ya kutoka Nairobi kuelekea Naivasha na kadhalika.

Aliyekuwa waziri wa uchukuzi mwenye ushawishi na msimamo thabiti marehemu John Michuki alifaulu kuleta mabadiliko ya kufana katika sekta ya matatu. Alianzisha sheria maarufu zilizojulikana kama sheria za Michuki. Sheria hizi zilikusudia kuboresha usalama barabarani humu nchini. Kati ya mambo ambayo sheria hizi zilipiga vita, ni uchukuzi wa abiria kupita kiasi kilichoruhusiwa kisheria kulingana na ukubwa wa gari husika. Tabia ya kupakia mizigo na kubeba abiria kupita kiasi, imechangia sana katika kusababisha ajali barabarani. Hii ni kwa sababu uzito wa mizigo ukizidi gari,basi gari hilo huanza kuyumbayumba na kupoteza mwelekeo.

Madereva wanaoendesha magari kwa muda mrefu bila kupumzika pia huchangia kwa kiasi kikubwa ukosefu wa usalama katika barabara zetu. Ni wajibu wa waajiri kuwapa madereva muda wa kupumzika. Si ajabu kumwona dereva mmoja tu akiliendesha gari kutoka Garissa hadi Kakuma bila dereva msaidizi. Hii ni njia moja ya kuhatarisha usalama wa wasafiri katika barabara zetu.
Usalama wa barabara zetu unatiwa katika hali mbaya sana na madereva ambao wanaendesha magari huku wakiwa walevi chakari au wanatumia dawa za kulevya. Hivi majuzi nilipigwa na butwaa nilipokuwa nikitazama habari katika runinga moja nchini.

Dereva mmoja wa gari la uchukuzi katika barabara ya Jogoo, aliliacha gari likiwa linaenda na kutimua mbio kukwepa maafisa wa trafiki waliokuwa wakiwanasa madereva walevi. Ilimbidi askari mmoja kulifuata gari hilo na kushika breki zake ili kuokoa maisha ya abiria waliokuwa ndani. Aibu iliyoje kwa madereva walevi? Ajali pia husababishwa iwapo magari hayafanyiwi ukarabati au kubadilisha vyuma vilivyoharibika, kuchakaa au kuvunjika. Hivi majuzi kulikuwa na ajali mbaya sana iliyotokea katika barabara ya Waiyaki kwa sababu dereva wa trela lililohusika alishindwa kudhibiti breki za trela hilo. Ghafla bin vuu trela hilo liligongana ana kwa ana na basi la abiria na kuwaua wasafiri wengi sana.

Matumizi ya simu za rununu pia imechangia pakubwa katika kueneza maafa kwenye barabara zetu.Utawaona baadhi ya madereva wakipokezana jumbe fupi na kupokea simu huku wakiendesha magari.Tatizo hili ni sugu mno hususan katika magari ya kibinafsi yanayoendeshwa na mabarobaro. Si ajabu kuwaona baadhi yao hata wakiacha usukani wa gari ili kugotana.
Ni jukumu la kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa usalama wa barabara zetu unazingatiwa ili kuepuka maafa katika sekta hii ya usafiri.

Swali

a) Jadili visababishi vya ukosefu wa usalama barabarani alama (10) maneno 100

Matayarisho

Jibu

b) Bila kupoteza maana fupisha aya ya kwanza (alama 5)

Matayarisho

Jibu

Matumizi ya lugha **alama 40**

a. Andika sauti moja sighuna ambayo ni kikwamizo cha ufizi. (ala1)

_____

_____

b. Eleza maana ya sauti mwambatano (ala1)

_____

_____

c) Kwa kutoa mifano, onyesha tofauti kati ya silabi tatanishi na sauti tatanishi (ala2)

_____

_____

d) Tunga sentensi iliyo na muundo ufuatao. E+N+U+N+T+N+V+E. (ala2)

_____

_____

e) Onyesha iliko shadda katika sentensi:
Kijiko ki juu ya meza. (ala1)

f) Mofimu tegemezi ni nini? (ala1)

_____

_____

g) Bainisha mofimu katika neno; watamnywea (ala2)

_____

_____

h) Tunga sentensi iliyo na kiambishi tamati cha amri. (ala1)

i) Tunga sentensi ukitumia kiambishi ka kuonyesha hali ya kufanyika (ala1)

j) Tunga sentensi kwa kutumia kiunganishi 'mintarafu ya' (ala1)

k) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha kukinzana (ala1)

l) Nomino katika ngeli ya U-ZI huchukua maumbo tofauti katika umoja na wingi. Fafanua kauli hii kwa mifano yoyote minne. (ala2)

m) Kanusha katika wingi. (ala1)

n) Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari
Ubora wa kazi zao ulifichika baada ya kuanzishwa kwa mradi ule. (ala2)

o) Tunga sentensi zinazobainisha matumizi mawili ya neno HAZINA. (ala 2)

p) Unda kitenzi kutokana na nomino vifuatavyo: (ala 2)
zawadi- .
sijida -

q) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi tegemezi (ala 1)

r) Tumia mzizi '- enye' katika sentensi kama:
Kivumishi , Kiwakilishi . (ala 2)

s) Eleza maana ya kirai (ala2)

t) Andika katika usemi halisi.
Mkuu wa polisi alilalamika kwamba vibanda hivyo vilikuwa vikitumiwa kulanguzia dawa za kulevya. (ala1)

u) Eleza maana ya kijalizo (ala 2)

v) Bainisha viwakilishi <u>vinne</u> katika sentensi hii. (ala2)
Aliwaletea saba.

w) Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha idadi isiyo dhahiri katika ngeli ya U-I. (ala2)

x) Andika kisawe cha neno <u>chupi</u> (ala 1)

y) Tunga sentensi moja yenye viungo vifuatavyo vya sarufi. (ala2)
Kikanushi cha ngeli ya A-WA nafsi ya kwanza
Kikanushi cha wakati ujao
Kiwakilishi, nafsi ya pili wingi
Mzizi wa kitenzi cha silabi moja-kunywa

Mnyambuliko wa kitenzi kauli ya kufanyia

z) Tunga sentensi moja ukionyesha shamirisho kipozi, kitondo, ala na chagizo (alama2)

ISIMU-JAMII **(alama 10)**

Eleza maana ya lugha (alama 1)

Tofautisha kati ya pijini na krioli (alama 2)

Jadili sifa tatu za pijini. (alama 3)

Eleza maana ya lingua franka. (alama 1)

Eleza maana ya diglosia (alama 1)

Eleza changamoto mbili zinazokumbuka maenezi ya Kiswahili nchini (alama 2)

Kila la kheri. S.Ngige